TANGAZO LA SERIKALI NA.193 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA KIMBARAGE YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Kimbarage ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la Upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Njombe .

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Mpaka unaanzia kwenye majira – nukta 691802.7754MS, 8965837.4961KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.203 hadi kwenye majira – nukta 692005.5955MS, 8965823.4387KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa kufuata bonde kwa umbali wa kilomita 0.334 hadi kwenye majira – nukta 692138.2308MS, 8965516.4038KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.209 hadi kwenye majira - nukta 692129.3373MS, 8965307.0359KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.214 hadi kwenye majira - nukta 692342.8184MS, 8965299.1335KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya mtaa lilipo soko la mbao kwa umbali wa kilomita 0.211 hadi kwenye majira – nukta 692365.1756MS, 8965088.8772KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa kufuata barabara ya Mfereke kwa umbali wa kilomita 0.202 hadi kwenye majira – nukta 692553.6759MS, 8965160.8374KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.235 hadi kwenye majira – nukta 692631.8102MS, 8964939.0142KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.457 hadi njiapanda ya barabara ya Magoda kwenye majira – nukta 693080.7356MS, 8965023.2839KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Magoda kwa umbali wa kilomita 0.769 hadi njiapanda ya barabara ya Magoda na bonde la Nyikamtwe kwenye majira – nukta 692838.4849MS, 8964293.013KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata bonde la Nyikamtwe kwa umbali wa kilomita 0.89 hadi barabara ya Mfereke kwenye majira – nukta 692021.5315MS, 8964369.2458KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya Mfereke kwa umbali wa kilomita 0.241 hadi njiapanda ya barabara Mfereke na bonde kwenye alama yenye majira – nukta 692110.2562MS, 8964593.4246KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata bonde kwa umbali wa kilomita 0.782 hadi kwenye majira – nukta 691553.3489MS, 8965088.5748KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.244 hadi kwenye majira – nukta 691781.0125MS, 8965176.0935KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.72 hadi ulipoanzia”.

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*